# KUWA WASHIRIKA WA TABIA YA KIMUNGU

*2Petro 1:3-4* *Kwa kuwa uweza wake wa uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua Yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo tupate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo. Wewe hujaokolewa bado mpaka umepokea Roho Mtakatifu. Biblia ilisema hivyo. Baada ya Petro kuwa ameokolewa na kutakaswa, akapewa nguvu za kutoa pepo wachafu, na kuhubiri injili. Yesu kwa wazi alimwambia hujaongoka, mpaka alipojazwa na Roho Mtakatifu. Na Yeye akamwambia "Nawe utakapoongoka waimarishe ndugu zako". (Luka 22:31-32). Hiyo ilikuwa usiku ule wa kusalitiwa, kwamba alikuwa bado hajaongoka. Na hakuna mtu ambaye ameongoka kweli kweli mpaka awe amebadilishwa, na amekufa kwa yeye mwenyewe, na Roho Mtakatifu ana utawala juu ya mtu huyo. Hawapendi kulifanya hilo.

Sasa, Roho Mtakatifu hatakosa kujiheshimu kwa mtu mmoja, na ajiheshimu mwenyewe kwa mwingine. Atamfanya kila mtu aje katika tabia yake (ya Kimungu), kwa sababu ni Roho anayekuongoza. Anakuleta ukubaliane na tabia yake.

Humfanyi Yeye akubaliane na tabia yako; Anakufanya ukubaliane na tabia Yake. Na Roho Mtakatifu anakufanya uishi na ufurahie kufanya hivyo. Oh jinsi unavyofurahia kuyaacha mambo ya dunia, Pale Roho Mtakatifu anapokuja ndani. Jinsi anavyokuosha na kukusafisha wewe 1Yoh 3:3 na anavyoweka shauku ndani yako ya kumfuata Yeye na kiu, na njaa ya kupata zaidi, unaoga tu pale, Analeta uhalisi.

Na huwezi ukamfanya mtu alione Neno la Mungu mpaka tabia yake ya asili imegeuzwa. Na tabia ya asili inapogeuzwa kutoka kile alicho na kuwa Mwana wa Mungu na Roho Mtakatifu anakuja ndani yake …….

Tafadhali elezea tofauti kati ya roho na nafsi. Vyema sasa hilo ni gumu. Lakini jambo la kwanza wewe ni mwenye sehemu tatu kama vile Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni vyeo vitatu vinavyomhusu mtu mmoja. Ambaye ni Yesu Kristo. Na wewe u nafsi, mwili na roho na inachukua sehemu hizo tatu kukufanya wewe; ikiwa ni sehemu moja tu, hiyo siyo wewe inachukua sehemu hizo tatu kukufanya wewe.

Kama nilivyosema siku iliyotangulia. Huu ni mkono wangu; hiki ni kidole changu; hii ni pua yangu; haya ni macho yangu, lakini mimi ni nani? Mimi ni nani ambaye anao huo? Ni hiki kilicho ndani yangu; hiyo ni ule ufahamu au akili yangu.

Kama macho haya, kama mikono hii, kama mwili huu ungesimama hapa kama ilivyo leo, bado ninge ………… Mwili wangu ungekuwa hapa. Lakini mimi ningekuwa nimekwenda. Mimi ni nani. Vile vyovyote nilivyo ndani yangu vitakuwa vimekwenda. Hivyo ndiyo sehemu ile ambayo ni roho. Nafsi ni asili ya roho, kwamba Roho Mtakatifu anapokuja ndani yako, hafanyi chochote isipokuwa Anabadilisha roho yako kuwa nafsi nyingine. Na hiyo nafsi ni asili nyingine inayokuwa ndani ya roho hiyo. Kwa hiyo nafsi ni asili ya roho.

Kwanza ulikuwa mchoyo, na mwovu, na chuki na magombano; sasa una upendo, uko mtamu, mkarimu na ……. Unaona ile tofauti? Ni ile asili yako. Tunaweza ………. Nitaita hivi. Ni nafsi yako iliyokuwa imebadilishwa. Ile nafsi ya zamani imekufa (Ezekieli 18:20), na nafsi mpya ambayo ni asili mpya imezaliwa ndani yako.

Bongo yako siyo akili yako, ni roho iliyo ndani yako hiyo ndiyo akili yako unaona? Ubongo wako ni mkusanyiko wa aina ya nyama laini na chembe chembe hai n.k. hauna akili wenyewe kama ulivyo. Kama ungekuwa nayo, ili mradi umelala pale, kama ulikuwa umekufa au umekuwa hai ungekuwa unafanya kazi. Unaona? Lakini siyo bongo yako, ni roho iliyo ndani yako. Na nafsi yako ni asili ya roho. Hiyo ni nafsi ya roho ambayo inatawala – roho inayotawala mwili wako (Yakobo 3:1-8) unaona? Angalia tuko hapo.

Sasa nafsi ya mtu siyo mwili wa mtu, hiyo ni nafsi na nafsi ni kitu fulani ambacho ni asili ya roho, na halafu asili ya mtu ….. Aliposema, "Tumekufa" maandiko kwa wazi yanatuambia kwamba tumekufa, na uhai wetu umefichwa ndani ya Mungu kwa Kristo, na kutiwa mhuri wa Roho Mtakatifu (Kolosai 3:1-4) Sasa siyo kuwa mwili wako umekufa. Siyo kuwa roho yako imekufa. Ni ile asili ya roho yako iliyokufa unaona? Ile asili ambayo ni nafsi. Asili ya nafsi yako ni Mungu. Kama umezaliwa mara ya pili (Tito 3:4-7); kama siyo basi ni ya dunia.

Kila kitu chenye mwanzo, kina mwisho, kwa hiyo njia pekee uwezayo kuwa nayo kupata uzima wa milele ni kuwa na uhai ambao hauna mwanzo. Ndio hapo sasa maisha yako yameanza pale ulipozaliwa. Wakati Mungu alipopulizia pumzi ya uhai ndani ya pua nawe ukawa nafsi iliyo hai hapo sasa ndipo ulianza (Mwanzo 2:7) Lakini wakati ……… ile asili ambayo ilikuwa ndani yako, kwa asili ulikuwa ni wa dunia, aliyefarakana na Mungu (Waefeso 2:1-3).

Lakini ile nafsi iliyo pale, hiyo nafsi ndiyo ambayo Mungu anaifanyia kazi. Unaona, kama angeweza tu kuipata hiyo asili ya roho ikubaliane na Yeye, hiyo asili inakufa. Ile asili na upendo kwa dunia imekufa na mambo ya dunia yamekufa; kwa sababu kama unaipenda dunia au mambo ya dunia, upendo wa Mungu haumo ndani yako (1Yohana 2:15-17) unaona?

Na mtu ni lazima azaliwe mara ya pili, ili hiyo asili ipate kufa na asili ya Mungu inakuja ndani yako (1Petro 1:22 – 23) na Mungu ni pekee tu ambaye hana mwanzo na hawezi kamwe kuwa na mwisho.

Hiyo ndiyo maana tunabatizwa kwa Jina lake ili kwamba tuinuke kwa Jina lake, katika kifo chake, katika kufufuka kwake, kwamba tunainuka tukishuhudia kwa ulimwengu kwamba tuna maisha mapya, kwamba yule mtu wa kale amekufa. Tumezika ile asili ya zamani (Warumi 6: 3-6).

Unaona, ile asili ya kwanza imeondoka, na sasa tu wa asili Yake. Anaishi ndani yetu, na hatufanyi mapenzi yetu, tunafanya mapenzi yake (Luka 6:46-49). Hatufikirii mawazo yetu, nia ndiyo inayofikiri. Nia iliyokuwa ndani ya Kristo Yesu iko ndani ya kila mwaminio (Wafilipi 2:5-11) unaona? Iko nafsi pale na hiyo ndiyo tunayoizungumzia sasa, hiyo ndiyo sehemu ninayofikiria sasa, kwamba iko nasi, hiyo nafsi.

Mwangalie Paulo, Paulo alikuwa mwanatheolojia mkuu. Lakini alipokutana uso kwa uso na Neno, Yesu lilimhuisha. (Matendo 22: 1- 16) Akawa hai haraka sana kwa kuwa alikuwa amekusudiwa hivyo. Alikuwa sehemu ya hilo Neno, ilikuwa ni asili yake. Kulia kote kwa kuku wa kanisa alilokuwa, hakukuwa na madhara juu yake. Alikuwa ameona Neno. Ilikuwa sehemu yake. Yeye alikuwa ni tai. Hakuwa kuku alikuwa tu bandani pamoja nao. Lakini kwa kuanzia Yeye alikuwa ni tai.

Nimesikia hadithi ndogo inayofanana na hiyo, natumaini halitaonekana la kipuuzi, juu ya bata mdogo akiwa amezaliwa chini ya kuku wakati mmoja. Hakuweza kuelewa. Alionekana mdogo na kichekesho, aliyetofauti na hakuelewa mavumbi na kadhalika. Walikuwa wanacheza ndani ya banda. Lakini siku moja kuku yule aliongoza vifaranga hivyo nyuma ya banda, akapata harufu ya maji. Kwa nini, alianza kutembea kuelekea maji kwa bidii kadiri alivyoweza. Kwa nini? Hajawa katika bwawa la maji hata siku moja. Hajawa kwenye maji. Lakini Yeye alikuwa bata kwa kuanzia. Alichopaswa kufanya ni kujitambua tu.

Hivyo hivyo ndivyo mwaminio alivyo. Kuna kitu ndani yake, anapokutana na Mungu uso kwa uso, anajitambua. Ile mbegu iko ndani yake, nayo inahuishwa. Jamani, hiyo ni kweli, na yeye anakimbia mbali kutoka kwenye mambo ya dunia. Yanakuwa yamekufa kwake oh mimi, nakumbuka sisi sote tuna maisha yetu yaliyopita katika mambo hayo ya dunia. Lakini mara tunaposhikilia kile kitu halisi, kitu fulani kilichotuhuisha sisi, ile mbegu ndogo ambayo inakuwa hai (Matayo 13:37-38, Luka 8:11), hapo sasa mambo yote ya dunia yanaoza hapo hapo. Hatuna tena shauku na mambo hayo.

Na walinisikia mimi nikisema ushahidi wa kuwa na Roho Mtakatifu siyo kuzungumza kwa lugha …….. na siyo ……. Lakini nilimshauri yule mtu amuulize Mungu ili ampe kunena kwa lugha au kutabiri, kwa sababu inategemea asili.

Kitu cha kwanza, nilienda kwa yule mtu nikafahamu mahali alipozaliwa, na wamezaliwa chini ya ishara gani, na naweza kueleza kuzaliwa kwao kulivyokuwa. Ni katika njia ipi ambayo asili ya kawaida inawaweka katika mstari wa aina fulani. Sasa wanapozaliwa mara ya pili, wanakuwa hapa kwenye asili nyingine na halafu unapotafuta kwenye asili hii, ule utu wa ndani, katika dhamiri dhamiri ya ndani ……….. Dhamiri ya nje inakuvuta upande mmoja wa njia; hiyo ni asili yako ya kuzaliwa. Hapo sasa watafanya kitu fulani ambacho kinawaweka mahali gani? Katika migawanyiko minne, inawaweka kwenye hali iliyogawanyika. Hawajui chakufanya, watasema, Bwana anataka mimi nifanye hivi.

Kule ndani "Oh najua hiyo inakubaliana na mandiko" na wataanza kulifanya na jambo la kwanza unajua, shetani upande huu mmoja atawaonyesha wao kila aina ya makosa ndani yake. Nao wanasema vyema, nadhani unaona, unaona? Wanamsikiliza shetani unaona? Inabidi uchukue kile kitu fulani cha ndani, kile ambacho kiko ndani yako ambacho ni maandiko. Na usimwache shetani asimame popote. Huo ni wajibu wake kusimama pale kukupiga wewe kama hivyo. Lakini usimsikilize yeye.

Na mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu anakuwa hua wa Mungu, asili yake, badiliko lake, maumbile yake. Ndiyo Bwana. Wewe uweke roho wa hua ndani ya kunguru, hatakaa kamwe katika mzoga uliokufa. Kama angelikutana nao kwa makosa, hakika ataondoka mbali haraka; hawezi kulistahimili hilo.

Na mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu, hawezi kulivumilia hilo. Anaweza akaangaza ndani ya Chumba cha baa wakati mwingine, lakini atatoka pale haraka. Mwanamke anaweza kumdanyanya, akamgeuza huku kuangalia, lakini ategeuza kichwa chake tena. Ataondoka pale haraka, kwa nini? Yeye ni hua (njiwa). Hiyo ni kweli. Hutamdanganya Yeye, kwa sababu anajua. "Kondoo wangu wanaijua sauti yangu na hawatamfuata mgeni" (Yohana 10:27-30) Yeye ni hua kwa kuanzia. Hicho ndicho ninachozumgumzia kitu fulani halisi kinachoweka nanga pale.

Siku moja Yesu alikuja akitembea kule akasema, "Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" Yule kondoo, upatanisho sahihi (Yohana 1:29-34; Matayo 3:13-17), Pale anakuja yule ambaye kila mwanakondoo

kutoka bustani ya edeni hadi hapo alieleleza, mtu wa kawaida akitembea chini mtoni.

Wakasema "Yohana, umejuaje hilo? Sikuona kitu hata kimoja cha tofauti" Lakini ninashuhudia; niliona Roho wa Mungu akishuka kama hua na sauti ikisema, "Huyu ni mwanangu mpendwa ambaye nimependezwa kukaa ndani yake".
Mwangalie Hua na Mwanakondoo. Unaona? Ndiyo. Vipi kama ingekuwa ni mbwa mwitu amesimama pale? Vyema, yule Mwanakondoo asingekaa juu yake ………. Hapana nia Hua ……… Mungu amejieleleza mwenyewe na Hua, Ndege mnyenyekevu kuliko ndege wote wa anga, Mwanawe amemueleleza na Mwanakondoo, mnyama mpole sana kuliko wote duniani. Unaona, ndege msafi wa anga, siyo kunguru, mwewe, lakini ni Hua; siyo nguruwe. Lakini Mwanakondoo. Asili nyingine yoyote visingeweza kuungana pamoja.

Na angalia yule Hua alipokuja kwa Mwana kondoo, alimuongoza. Siyo kwa namna aliyotaka, lakini kwa njia Baba aliyotaka kumuongoza Yeye (Yohana 5:19 – 30). Hivyo ndivyo Mwanakondoo halisi alivyo leo. Oh hujui kwamba Mungu anaongoza tu kwa Neno lake? Hilo ndilo nguzo yake.

Angalia hakuna ambacho kingefanyika, lakini Yohana alisema, "Wengine wote hawakuiona lakini ninashuhudia niliiona huko akitangaza "Tazama Mwanakondoo wa Mungu achukuaye dhambi ya ulimwengu".

Tazama yule Hua mdogo anavyoruka. Ni ndege wa tofauti jinsi gani. Unaona? Yeye hana nyongo yoyote, hawezi kula kama kunguru awezavyo. Unaona? Yeye hana nyongo ndani yake. Hahitaji kuoga ndani ya maji, kwa sababu ana kitu fulani ndani yake; kinachomsafisha kutoka ndani kuja nje.

Hivyo ndivyo mkristo alivyo. Hivyo ndivyo Mungu alivyojiwakilisha, katika Hua unaona? Kwa sababu ndani ya ……… Yesu aliwakilishwa na Mwanakondoo. Siku zote kwenye mambo ya asili utamuona Mungu. Na Mungu ametulinganisha na kondoo ambaye apaswa aongozwe (Yohana 10:1-30). Je uliweza kuona pale, kwamba hua akija juu ya Mwanakondoo, kumuongoza Mwanakondoo na ilimuongoza Yeye kwenye machinjo yule …….. yule Hua, sasa kama yule Mwanakondoo …. Yule Hua asingeweza kushukia juu ya mnyama yoyote mwingine kwa sababu wote wanapaswa kuwa na asili moja. Unaona? Kama Hua angetua juu ya mbwa mwitu naye angeng'aka au kubweka, yule Hua angeruka na kuondoka.

Vyema ni sawa sawa na ilivyo sasa. Njia zetu mbaya, Roho Mtakatifu anaruka na kwenda zake. Lazima viwe na asili moja. Ndege wa angani yule Hua; Mnyama mpole sana duniani Mwanakondoo, wanaweza kukubaliana pamoja. Na Roho Mtakatifu anapokuja juu yetu na kutufanya sisi viumbe vipya (2Kor.5:17), Hapo anaweza kutuongoza sisi. Lakini tukijaribu kuishi maisha yale yale ya zamani, haiwezi kutenda kazi, haiwezi kutenda kazi.

Kijana mdogo aliniuliza mimi siku ile nyingine, alisema unafikiri unaweza – naweza kumuoa msichana yule fulani. Ndugu Branham? Nikasema ni kwa kiasi gani wewe unamfikiria yeye? Akasema "Oh jamani ninampenda sana yeye" Nikasema; vyema kama huwezi kuishi bila ya yeye, ni vizuri umuoe basi lakini kama unaweza kuishi bila yeye usimuoe kwa hiyo ………. Lakini kama litaenda kukuua wewe, ni vizuri uendelee na uweze kumuoa. Nikasema na sasa nilichokuwa ninajaribu kumuelezea ni hiki kama unampenda sana …….. sasa, wakati huu kabla hamjaoana, kila kitu ni kizuri na cha kufurahisha. Lakini baada ya kuoana hapo mahangaiko na majaribu ya maisha yanaingia. Hapo ndipo mnapaswa kuwa mnapendana kweli kiasi kwamba mnaelewana mmoja na mwingine. Unapovunjwa moyo naye au anapovunjwa moyo nawe bado mnaelewana mmoja kwa mwingine.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa Kristo. Unaona inabidi tuwe katika upendo naye mpaka tunapoomba kitu fulani Naye kama hatupi, haitusogezi hata kidogo unaona? Kwa nini? Na njia pekee tu uwezayo kufanya hivyo ni kuwa mshirika wa tabia yake ya Kimungu. Kwa hiyo unaweza kuelewa sababu kwa nini Yeye hakupi hicho wewe.

Ushirika wa tabia ya Kimungu. Na angalia hapa "mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa" – kukimbia hayo (2Petro 1:3-4). Unaona linamhusu nani? Ni kwa Kanisa. Wale walio ndani ya Kristo wameinuliwa juu ya mambo hayo, siyo kwa kujiinua wenyewe, lakini Kristo amewainua juu.

Na kama una Roho wa Kristo ndani yako, wewe ni wa juu mbinguni. Hivyo ni mgeni hapa (1Petro 1:17-23). Lakini unayo asili ya mahali pale unapotoka. Hicho ndicho ninachojaribu kuzungumza.

Mrumi akija hapa naye atakuna kichwa chake na Mjerumani akija hapa; na Mwamerika akienda pale ni nini? Una roho ya zile nchi ambako umetokea. Hiyo ndiyo inayotufanya sisi tofauti sana na watu wa dunia. Umetoka juu (Yohana 17:6-14) wewe umezaliwa; ni mwenyeji wa ufalme mwingine (Wafilipi 3:20 – 21) unaamini hilo? Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, ni kukufanya wewe kuwa mwenyeji wa ufalme wa Mungu..

Na kama wewe ni mwenyeji wa ufalme wa Mungu, inakufanya utende vipi? Kama Mungu afanyavyo katika ufalme wake. Sasa, Mungu anafanya nini katika ufalme wake? Ni utakatifu, ni haki, usafi wa mawazo, usafi wa nia, nguvu na upendo, kuwaendea waliopotea, kuwaponya wagonjwa, kufanya miujiza, kufanya mambo

makuu. Hivyo kwa dunia unaoneka kuwa punguani; wanasema "Watu wale vichwani mwao wamepungukiwa" unaona? Lakini wewe ni mwenyeji wa ufalme.

Kwa hiyo, tu wasafiri na wageni hapa; haya siyo makao yetu ya kudumu. Lakini tunautafuta mji ujao ambaye mwenye kuubuni na kuujenga ni mungu (Waebrania 11:10) kwa hiyo, unapozaliwa kutoka juu, unaye Roho Mtakatifu akija kwako kutoka kwa Mungu, hivyo anabadilisha asili yako. Haijalishi dada yako, mama yako, rafiki yako mkuu anaweza kuvalishwa njia hii; Lakini Mkristo aliyezaliwa na Roho wa Mungu amezaliwa kutoka juu na Roho zao ni za ufalme mwingine oh, ninalifurahia hilo. Urahisi wa Roho Mtakatifu, kumfuata Yeye, kumuangalia Yeye, jinsi anavyotenda inakufanya utende hivyo.

Kabla Mungu hajashuka chini katika utu wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Kristo akija chini na kukaa katika moyo wa mwanadamu, ambao kwanza lazima utubu. Lazima ubatizwe kwa maji katika Jina lake ili kuonyesha yeye ni mali ya nani (Matendo 2:37-41). Halafu inabidi uoshwe kwa damu ya Yesu. Na hapo sasa Moto mtakatifu na Roho Mtakatifu kutoka kwa Mungu anashuka chini na kuteketeza kabisa kila shauku ya dhambi, tabia zote za asili ya dunia. Na kwa hiyo, Yeye afanyaye dhambi kwa makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa kweli ………. (Waebrania 10:26-27)

Halafu tena Biblia ilisema, haiwezekani, kwa mtu ambaye amezaliwa na Mungu kutenda dhambi; hatendi dhambi. Hakuna njia kwa yeye kutenda dhambi (1Yohana 3:9; 5:18). Awezaje kuwa mwenye dhambi na aliyekombolewa wakati huo huo? Nawezaje kuwa katika duka la rehani na kuwa nje ya duka la rehani wakati huo huo? Unaona? Oh Ametukomboa sisi kwa Damu (Waefeso 1:7); kwa Roho wake Ametusafisha sisi, na tena akaja kukaa ndani yetu (Waefeso 2:19-22). Kanisa, siyo madhehebu sasa, Kanisa.

Damu takatifu iliyoumbwa na Mungu, Damu, uhai, Uumbaji wa Mungu; Yesu ni mwanzo wa uumbaji wa Mungu (Wakol. 1:13-16) Oh mimi. Unaliona hilo, Mungu akifanywa katika uumbaji ……… Yeye alikuwa Roho.

Biblia imesema Yeye ni mwanzo wa uumbaji wa Mungu. Ameanzaje? Ndani ya tumbo la mwanamke, ambalo ni nini?

Ni kwa namna gani watu hawa vipofu hawawezi kuona uzao wa nyoka hapa hapa. Unaona? Hawa aliwekwa hapa duniani, na hata kabla shetani hajamgusa mwanamke au chochote, Mungu aliwaambia wao, "Zaeni na mkaijaze nchi" (Mwanzo 1:28). Hiyo ni sahihi. Lakini shetani anakuja ndani hapa, na kama huyo (Kaini) angekuwa mwana wa Adamu, ambapo Adamu alikuwa ametoka moja kwa moja kwa Mungu na unachukua tu asili ya wazazi wako. Na unapozaliwa mara ya pili unachukua asili ya wazazi wako mbinguni. Na wazazi wako wa mbinguni ni sehemu ya Neno au Neno ni sehemu ya wazazi wako, na utalipingaje usimamie dhehebu?

Na mtu ambaye amezaliwa na Mungu, Mwana wa Mungu anapaswa kuwa na asili ya Mungu. Anapaswa awe kama Mungu. Yeye ni sehemu ya Neno la Mungu.

Nukuu za kiingereza:
Uhalisi wa Mungu usioshindwa aya 75/76 mabirika yavujayo (64-0726E) Aya 65, Maswali na majibu (61-1015m) swali na. 157 cod uk 676.
Nafsi zilizoko kifungoni sasa uk. 6-9/Mungu aliye mwingi wa rehema aya 51-53. Maswali na majibu (64 – 0830m Cod uk 1075 Aya 59-61, Waebr. Sura no. 7 uk 266/
Kwa nini ilikuwa wachungaji aya 199 – 204; Uongozi (65 – 1207)
Aya 93 – 95, Kimo cha mtu mkamilifu, uk 8 – 9 – 13.
Kwa nini tumepewa Roho Mtakatifu Aya 147-149
(Dhoruba) zinazokuja Aya 84 Makao ya baadaye uk. 18, 45
Muungano wa siri wa Kristo na Bibi harusi uk 34

Jiwe la kujengea la kiroho no. 141 kutoka Neno la saa hii iliyokusanywa na Gerd Rode Wald, Friedenstr. 69,D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya harka itaizunguka dunia. Zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyoteuliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk. 724).

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*